

## BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA



### UTARATIBU WA KUHAMIA MTAALA WA ELIMU YA TANZANIA KWA WANAFUNZI WANAOSOMA MTAALA WA ELIMU USIO WA TANZANIA

Mwanafunzi yeyote ambaye amesoma Mtaala wa Elimu ambao sio Mtaala wa Elimu ya Tanzania ni **lazima** afanyiwe ulinganifu kabla ya kujiunga na kuendelea na masomo ya ngazi husika ya Elimu hapa Tanzania. Ufuatao ni utaratibu wa mwanafunzi kuhamia Mtaala wa Elimu ya Tanzania kwa Mitihani inayoendeshwa na Baraza la Mitihani la Tanzania.

#### 1. WANAFUNZI WANAOSOMA MITAALA YA NJE KATIKA SHULE/VITUO VILIVYOPO NDANI YA NCHI.

Baraza la Mitihani litahitaji nyaraka zifuatazo ili kufanyika kwa ulinganifu huo;

a) Fomu ya ulinganifu iliyojazwa kikamilifu.

Kupata fomu hiyo, ingia kwenye tovuti; [www.necta.go.tz](http://www.necta.go.tz) kisha kwenye 'Forms' pakua fomu ya 'Equation of Curriculum' iliyoopo kwenye kasha (Folder) lililoandikwa 'Equivalence'.

Maombi yatumwe kwa: **Katibu Mtendaji, Baraza la Mitihani la Tanzania, S.L.P 2624, Dar es Salaam, E-mail:**[esnecta@necta.go.tz](mailto:esnecta@necta.go.tz)

b) Barua ya uthibitisho kutoka shule/taasisi aliyokuwa akisoma mwanafunzi ikionesha;

- (i) Anuani kamili ya taasisi husika
- (ii) Nakala rasmi ya kadi ya maendeleo Kitaaluma kwa wanafunzi wanaoendelea na masomo katika ngazi husika **au** Cheti cha Kitaaluma kilichotolewa na Bodi husika kwa wanafunzi wanaojiunga na ngazi ya juu kielimu.
- (iii) Picha ya mwanafunzi anayeombewa ulinganifu. Picha igongwe muhuri wa taasisi.
- (iv) Nakala ya nyaraka ya usajili kutoka Bodi ya Mtaala husika kuendesha mafunzo tajwa.
- (v) Nakala ya Kibali cha Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa taasisi kuendesha Mtaala wa Bodi husika.

#### 2. WANAFUNZI WANAOSOMA MITAALA YA NJE KATIKA VITUO VILIVYOPO NJE YA NCHI

Kuhusu uhamisho wa mwanafunzi wa shule za msingi anayeingia Nchini, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inaelekeza kuwa azingatie utaratibu ufuatao;

a) Mwanafunzi atapokelewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia/kwa kuonesha barua toka Wizara ya nchi anakotoka, barua hiyo isainiwe na kugongwa muhuri na mamlaka husika. Barua hiyo iwe na vitambulisho vifuatavyo;

- (i) Taarifa ya maendeleo ya mwanafunzi kuishia darasa alilopo.

- (ii) Vivuli vya hati ya kusafiria (passport) ya mwanafunzi na mzazi/mlezi.
- (iii) Taarifa ya usajili wa mwanafunzi.
- (iv) Kibali cha ukazi wa mwanafunzi kuonesha muda atakaokuwepo nchini.
- (v) Picha za passport

b) Afisa wa Wizara anayehusika atamjazia fomu mzazi/mlezi za kumtambulisha mwanafunzi Baraza la Mitihani ili afanyiwe ulinganifu. **Utaratibu huu ni kwa shule za Serikali na zisizo za Serikali.**

### **3. MAJIBU KUTOKA NECTA**

Majibu kwa mteja aliyekamilisha matakwa yote ya maombi ya ulinganifu kwa mujibu wa mwongozo huu yatakuwa tayari **ndani ya muda wa siku saba (07) za kufanya kazi** tangu siku nyaraka zilipopokelewa Baraza la Mitihani.